

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKO NA SERIKALI ZA MITAA

MKO WA DAR ES SALAAM

Anwani ya Simu:

Simu: 2203156/58

Fax: +25522203213

Tovuti: www.dsm.go.tz

Barua Pepe: ras@dsm.go.tz



OFISI YA MKUU WA MKOA

3 Barabara ya Rashidi

Kawawa,

S.L.P 5429,

12880 -DAR ES SALAAM.

Tanzania

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

HOSPITAL YA MAMA NA MTOTO CHANIKA ILIYOJENGWA KWA JITIADA ZA RC MAKONDA YAZINDULIWA RASMI.

Rais wa Shirika la Misaada la Korea Kusini KOICA Bi.Lee Mi Kyung amezindua Hospital ya Mama na Mtoto Chanika iliyojengwa kwa jitiada binafsi za Mkuu wa Mko wa Dar es salaam Mhe. Paul Makonda alietafuta wafadhili hao.

Ujenzi wa Hospital hiyo ya kisasa umegarimu zaidi Shillingi Billion 9.8 ambapo ndani kuna vyumba vya kisasa vya Upasuaji, vyumba vya Madaktari, Maabara,Chumba cha Mionzi, wodi ya wazazi,wodi ya watoto njiti, Theater, vyumba vya kujifungulia, ICU, Vyoo vya kisasa pamoja na nyumba za Familia 28 za madaktari ambapo ndani ya nyumba hizo kuna kila kitu.

RC Makonda amesema aliamua kutafuta wafadhili wa kujenga Hospital hiyo baada ya kuona kilio cha kinamama waliokuwa wakipoteza maisha na watoto baada ya kutembea umbali mrefu kufuata huduma za Afya.

Aidha RC Makonda amemuomba Rais wa KOICA kumjengea Hospital nyingine mbili kwenye Wilaya mpya za Ubungo na Kigamboni ili kusaidia maboresho ya huduma za afya.

Pamoja na hayo RC Makonda ameshukuru serikali ya Korea kusini kwa ufadhili wa hospital hiyo yenye hadhi ya kimataifa.

kwa upande wake Rais wa KOICA Bi. Lee Mi Kyung amesema shirika hilo litaendelea kushirikiana na serikali ya Tanzania katika masuala mbalimbali ya maendeleo huku akipongeza Tanzania kwa kudumisha amani tofauti na Mataifa mengine.

Uzinduzi wa Hospital hiyo umeenda sambamba na uzinduzi wa magari mawili ya kisasa ya wagonjwa (ambulance).

Imetolewa na:-

Kitengo cha Habari na Uhusiano

OFISI YA MKUU WA MKOA

DAR ES SALAAM

19/04/2018